AUSCO

Programu ya Maelekezo ya Kitamaduni nchini Australia

# Jamii za Waaustralia

Rahisi Kusoma

## Jamii za Australia hufanana vipi?



Nchini Australia kunazo aina nyingi za jamii.



Wanaweza kuwa tofauti sana na aina ya familia unayozoea.



Jamii za Australia zinaweza kuwemo pamoja na:


- baba, mama pamoja na watoto



- wazazi wa kabo pamoja na watoto wa kabo



- wazazi walezi pamoja na watoto



- ndugu na dada wanaojaliana



- wazazi wa kijinsia sawa



- babu na wazee wanaowatunza wajukuu



- mzazi mmoja anayewatunza watoto wake

# Jamii za Australia ni kubwa vipi?



Familia za Waaustralia zinaweza kuwa na ukubwa wowote.




Jamii nyingi zina mtoto 1 au watoto 2 pekee.



Jamii zinginezo zinaweza kuwa na watoto 3 au 4.



Baadhi ya jamii hawana watoto.




Wanawake wengi hawana mtoto mpaka wanapokuwa na umri wa zaidi ya miaka 30.

# Jamiii zilizopanuka



Jamii zilizopanuka zinaweza kuwepo na sehemu nyingi za jamii wanaoishi pamoja.



Jamii iliyopanuliwa inaweza kuwemo ni pamoja na:

- babu na bibi
- shangazi na wajomba
- binamu



Sio Waaustralia wote huishi katika jamii kubwa.


Wazazi ambao wanaozeeka kwa umri huishi:

- nyumbani kwao



- katika nyumba maalum ambapo hutunza watu wazee

# Kuoa na kuolewa



Wanaume na wanawake katika Australia wanaweza kuishi pamoja bila kuoana.




Hii huitwa uhusiano wa sheria-kawaida au kimapenzi.




Hii hutambulika kwa jamii na kisheria.




Katika Australia uko huru kuoa watu kutoka asili nyingine:


- rangi
- utamaduni
- dini

Wewe unahitajika kuwa na umri zaidi ya miaka 18 ili kuolewa.



Ikiwa wewe unao umri wa chini ya miaka 18 mahakama itaamua ikiwa wewe unaweza kuolewa.

Wewe unahitaji kuwa na sababu nzuri.




Ndoa ambayo imepangaliwa ni sawa katika Australia kama wote watu:

- wanataka kuoana
- wana umri zaidi ya miaka 18



Hakuna mtu anayeweza kulazimishwa kuoa.



Ndoa za kulazimishwa ni haramu.



Pia ni kinyume cha sheria kuwa mume au mke zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja.




Ikiwa watu 2 hawataki kuoana tena, wao wanaweza kupata talaka.


Talaka ni:




- kawaida
- inaitikishwa na jamaa

Ni kawaida kwa watu nchini Australia kufanya kuolewa tena baada ya kufanya talaka.

## Ajira na kazi



Wanawake wengi wa Australia wana ajira na kazi nje ya nyumbani.



Wanaume wengi wa Australia kusaidia na kazi ambayo inafanywa nyumbani.



Wao wanaweza:

- kufanya kununua chakula kulingana na mahitaji ya jamii
- kupika
- kusafisha
- kuwatunza watoto



Baadhi ya wanaume wanakaa nyumbani na kutunza watoto wakati wanawake kwenda kazini.



Vijana barubaru mara nyingi wana kazi za muda mfupi tu ili kuwasaidia:

- kupata pesa
- kujifunza ustadi mpya




Kuweko na kazi inaweza kuwasaidia hawa kupata:

- ujuzi kazini
- pesa
  - kwa ajili yao wenyewe
  - Ili kusaidia jamii yao kulipia bili

Australian Government
Department of Social Services

Inaletwa kwako na Shirika la Uhamiaji la Kimataifa kwa niaba ya Idara ya Huduma za Jamii nchini Australia

IOM • OIM